
Form C1

WIZARA YA MAJI

BODI YA MAJI BONDE LA WAMI/RUVU

# UTABIRI WA HALI YA WINGI WA MAJI KATIKA MTO RUVU KWA KIPINDI CHA SIKU 10 KUANZIA TAREHE 23 FEBRUARI HADI 04 MACHI, 2026







Imeandaliwa na;

Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu

P.O. Box 826, Morogoro—Tanzania

Phone: 0800114031 / 0800114032

E-mail: barua@wrbwb.go.tz

Website: www.wrbwb.go.tz

Februari, 2026


## 1. UTANGULIZI

### Yaliyomo


1. UTANGULIZI
2. ATHARI
3. UTABIRI WA HALI YA MAJI
4. USHAURI
5. HITIMISHO


Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu imeandaa na kuwasilisha utabiri wa wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa kuzingatia vituo vilivopo katika Catchment (**Kielelezo Na.1**) kwa kipindi cha kuanzia tarehe 22 Februari hadi 04 Machi, 2026. Utabiri huu unalenga kuwezesha wadau wa Mto Ruvu katika sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ujenzi, Viwanda, Utalii na Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira kufahamu mwenendo wa wingi wa maji katika mto huo.

waweze kujua hali ya mwenendo wa wingi wa maji. Aidha, utabiri huu umezingatia utabiri wa hali ya mvua na Joto zilizotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).




Kielelezo Na.1: Vituo vilivyotumika kufanya utabiri wa wingi wa Maji katika *Catchment* ya Mto Ruvu

### 1.1 ATHARI ZINAZOWEZA TOKEA


Uwezekano wa kiasi cha maji kuwa juu ya wastani wa muda mrefu (2009-2024), hali inaweza kusababisha yafuatayo;-

i. Uharibifu wa miundombinu na mali katika Mikoa ya Morogoro na Pwani.
ii. Kuchelewesha utekelezaji wa miradi ya ujenzi ikiwemo ujenzi wa mabwawa, Barabara, miradi ya maji katika Mikoa ya Morogoro na Pwani

## 2. UTABIRI WA HALI YA MAJI

Utabiri wa hali ya wingi wa maji katika Mto Ruvu umefanyika kwa siku kumi zijazo kuanzia tarehe 22 Februari hadi 04 Machi, 2026 kama inavyoonekana katika Jendwali Na. 1; -

**Jendwali Na. 1: Utabiri wa hali ya wingi wa maji Mto Ruvu.**

| **Jina la Mto** | **Utabiri wa Hali ya Wingi wa Maji** | **Kielelezo** |
|---|---|---|
| Ruvu | Utabiri unaonesha kuwa wingi wa maji unatarajiwa kuongezeka na kufikia kiwango cha juu ya wastani wa muda mrefu (2009–2024) kuanzia wiki ya kwanza ya mwezi Machi, 2026. Hali hii inachangiwa na uwepo wa mvua zinazoendelea kunyesha katika safu ya Milima ya Uluguru.<br>Aidha, kiwango cha maji kilichopo kwa sasa pamoja na matarajio ya siku kumi zijazo ni himilivu na kinatosheleza mahitaji ya sekta mbalimbali, ikiwemo mahitaji ya maji ya majumbani yanayohudumiwa na mitambo ya DAWASA ya Ruvu Juu na Ruvu Chini. Kwa sasa, mahitaji ya maji ni mita za ujazo sita (6) kwa sekunde. (**jendwali Na.1**). |  |

## 3. USHAURI KWA SEKTA MBALIMBALI

Bodi inapenda kuwashauri watumiaji wa Maji katika sekta ya Kilimo, Ujenzi, Madini, Utalii, Mifugo na uvuvi, Mamlaka na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira kuchukua tahadhari dhidi ya ongezeko la maji katika Mto Ruvu hali inayowezapelekea upotevu wa mali, uharibifu wa miundombinu na athari nyingine za kiuchumi na kijamii.

## 4. HITIMISHO

Bodi itaendelea kutoa taarifa ya mwenendo wa wingi wa maji kila baada ya siku kumi na kuwahabarisha watumiaji na Mto Ruvu ili waendelea kuchukua hatau za tahadhari dhidi ya kuongezeka/kupungua kwa wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa siku zijazo.